PRESS RELEASE
ISSUED BY INFORMATION SERVICES DIVISION
MINISTRY OF INFORMATION AND TOURISM
P. O. BOX 9142 DAR ES SALAAM TELEPHONE 20656
TIS

A/57/67
IT/I. 337

JANUARI 11, 1967.
(2.02 p.m.)

MWALIMU AFUNGUA MAJENGO
YENYE THAMANI YA PAUNI 460,000
MJINI BUKOBA

---

Rais wa Tanzania, Mwalimu Julius K. Nyerere, ambaye anaendelea na ziara yake ya Mkoa wa Ziwa Magharibi, leo (Januari 11) amefungua majengo mjini Bukoba, yenye thamani ya zaidi ya pauni 460,000.

Majengo hayo ni mtambo wa kutengenezea kahawa wenye thamani ya pauni 350,000; majumba ya Field Force yaliyogharimu pauni 94,349; mabweni ya shule ya Grewal Sekondari yenye thamani ya pauni 16,877 na Makao Makuu ya Tanu ya Mkoa yaliyonunuliwa kwa pauni 5,000.

Akiwa katika kiwanda cha kutengenezea kahawa, Rais alionyeshwa hatua mbali mbali za utengenezaji wa kahawa na Mkuu wa Kiwanda hicho, Bwana R. R. Welding. Ilisemekana kuwa kahawa itakayotengenezwa katika kiwanda hicho itaanza kutoka mwishoni mwa mwezi huu na sehemu kubwa yake itauzwa nchi za Ulaya ila sehemu kumi kwa mia tu ndio inatazamiwa kuuzwa Afrika Mashariki.

Katika Ofisi Kuu ya Tanu ya Mkoa, zitakuwemo ofisi zote za chama, Tapa, U.W.T. na Nuta.

Leo alasiri, Rais anatazamiwa kutembelea malisho ya ng'ombe (cattle ranch) huko Kitengule.

- MWISHO -